

**Karibuni shuleni tena!**

**Siku ya Jumatatu, Tarehe 27 Aprili, shule itafunguliwa tena kwa wanafunzi wa gredi 1-4 katika shule za manispaa ya Trondheim. Baada ya wiki kadhaa za masomo nyumbani, wengi wenu labda mnafurahia sana kukutana tena.**

## Mpendwa wazazi na walezi

Ni furaha kubwa kwamba sasa tunaweza kuanza kufungua tena shule zetu. Huu ni uamuzi wa serikali, kwa mujibu wa ushauri dhabiti kutoka kwa Taasisi ya Norwe Iliyo ya Afya ya Umma. Hii haimanishi kwamba Virusi vya Korona vimeondolewa nchini mwetu, lakini tuna udhibiti mzuri na tosha wa hali hii unaotuwzesha kurudia maisha yetu ya kawaida, ingawa bado ugonjwa huu uko katikati yetu. Kufunga shule na vituo vya utunzaji wa kila siku kwa njia ile tulizifunga, ilikuwa hatua ya dharura sana na hakuna aliyekuwa na uhakika wa matokeo ya hatua hizo wakati wa uamuzi huo.



Sasa tunajua zaidi. Tunajua kwamba wafanyakazi wa shule, walimu na wafanyakazi wasaidizi wamejitahidi sana kuhakikisha ukuaji wa wanafunzi katika masomo yao. Ubunifu na uwezo wa kidijitali umestawi sana. Wazazi na walezi wengi wamepata mtazamo mpya kabisa kuhusu kile shule haswa inapeana, kwa sababu walimu wamekuwepo katika nyumba zao.

Tunajua pia kuwa kufunga shule kuna athari ambazo zinaathiri watoto na vijana kwa njia tofauti. Shule ni zaidi ya mahali pa ukuaji katika masomo. Ni mahali pia pa urafiki, uchezaji, usalama na utunzaji. Kwa hivyo, ni muhimu sana kuwa shule zinaanza kufunguliwa tena.

Tuliwaalika wazazi na walezi ili watutumie maswali na tulipokea maswali mengi. Majibu yalipeperushwa moja kwa moja na kituo binafsi cha televisheni cha manispaa. Unaweza kutazama rekodi ya upeperushaji huo hapa:

<https://trondheim.kommunetv.no/archive/491>

Jopo lililojibu maswali lilihusisha Camilla Trud Nereid, Mkurugenzi wa Manispaa kuhusu Malezi na Elimu, Eva Elisabeth Belboe, Meneja wa Manispaa ya shule, Betty Johanne Pettersen, Afisa Mkuu wa Matibabu, manispaa ya Trondheim, Torgunn Reitlo Malmo, Mtaalam wa Saikolojia ya Kikliniki, na Trude Mathiesen, Mwalimu Mkuu.

Tutajumuisha baadhi ya maswali muhimu zaidi katika makala haya. Makala haya pia yatatafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza, Kipoli, Kisomali, Kifarsi, kitigrinya, Kiarabu, Kifaransa, Kihispania, Kitaki na Kiswahili.

Ninawakaribisha nyote shuleni tena siku ya Jumatatu, Tarehe 27 Aprili.

*Wako mwaminifu,*

*Camilla (Mkurugenzi wa Manispaa kuhusu Malezi na Elimu)*

### **Je, kwani nini ni shule za gredi 1-4 zinazofunguliwa tena pekee?**

Mkurugenzi wa Manispaa Camilla Trud Nereid: Hii ni kwa sababu wakati tunapaswa kuweka kipaumbele uzuiaji wa maambukizi, taratibu nyingi na maandalizi yanahitajika ili wafanyakazi na wanafunzi shuleni wawe salama. Tunaanza kwa wanafunzi wale wa umri mdogo kabisa kwa sababu hili ndilo kundi ambalo tunatatizika sana kulifikia kupitia mafundisho ya kidijitali. Taasisi ya Norwe iliyo ya Afya ya Umma ilipendekeza kufunguliwa tena kwa gredi 1-7 na lengo la serikali ni kukamilisha kufunguliwa tena kwa shule katika mwaka huu wa shule. Tunajali sana hasa wanafunzi wa gredi 10, ambao wako katika hali hii ngumu mwakani wa mwisho wa shule za sekondari za kiwango cha chini.

### **Je, makundi ya wanafunzi yatakuwa na saa tofauti za kupelekwa nyumbani?**

Mkurugenzi wa Manispaa Camilla Trud Nereid: Tumepanga ratiba rahisi kuhusu saa za kuanza, urefu wa siku ya shule na programu za kabla na baada ya shule (SFO). Ni muhimu kuendelea kuzungumza kwa karibu sana na shule husika, wafanyakazi, wawakilishi wa mfanyakazi na wawakilishi wa usalama na bila kusahau, wazazi na walezi ili kupata suluhisho bora kuhusiana na hili. Wakati huo huo, manispaa, kama mmiliki wa shule, lazima ihakikishe kuwa ubora wa programu unabakia mzuri, bila kujali suluhisho lililochaguliwa kwa karibu.

### **Je, kuhudhuria ni kwa lazima?**

Mkurugenzi wa Manispaa Camilla Trud Nereid: Kuna mahudhurio ya lazima shuleni katika nchi ya Norway, ambayo yanamaanisha kwamba wanafunzi lazima waende shuleni isipokuwa kuna sababu maalum za kutohudhuria. Masomo nyumbani ambayo yanapangwa na wazazi au walezi pia yanaruhusiwa, lakini tunapendekeza sana watoto waende shule.

### **Je, masomo kutoka nyumbani bado ni chaguo kwa wale ambao wanaweza kufanya hivi (k.m. wazazi walio likizoni ya wazazi au ambao hawafanyi kazi)?**

Mkurugenzi wa Manispaa Camilla Trud Nereid: Shule zitakapofunguliwa tena, wafanyakazi watotoa mafundisho kwa watoto watakaohudhuria shule. Tunashindwa kutoa mafundisho sambamba na seti moja tu ya wafanyakazi. Watoto wanaohitaji kukaa nyumbani kwa kipindi kirefu kutokana na ugonjwa, watapokea programu iliyobadilishwa. Hiki ndicho kiwango.

### **Je, mtoto wangu atarekodiwa kuwa hajahudhuria shule ikiwa tutaendelea na masomo nyumbani?**

Mkurugenzi wa Manispaa Camilla Trud Nereid: Ikiwa wazazi au walezi wamechukulia mikononi jukumu la elimu ya watoto wao, basi mtoto kamwe haendi shule na hivyo hatarekodiwa kuwa hajahudhuria. Ikiwa hali iko hivyo, basi wazazi au walezi hao sharti wawasiliane na manispaa na kuijulisha kuwa wamechukulia elimu mikononi mwao. Kutokuhudhuria kutarekodiwa ikiwa watoto walio na afya na wanaoweza kwenda shuleni watawekwa nyumbani, na wazazi au walezi hawajachukulia mikononi mwao jukumu la kuwafundisha.

### **Je, saa za kufungua shule na za programu za kabla na baada ya shule ni zipi (SFO)?**

Meneja wa Manispaa Eva Elisabeth Belboe: Ni muhimu manispaa ya Trondheim kulinda uzuiaji wa maambukizi na kupokea wanafunzi kulingana na miongozo ya kitaifa. Ili kufikia hili, huenda kukawa na haja ya kupunguza saa za programu za kabla na baada ya shule (SFO), na

tutaruhusu shule husika ziweze kuamua jambo hili kwa kushirikiana na wafanyakazi wao, baraza la watumiaji, kamati ya wazazi FAU), wawakilishi wa mfanyakazi na wawakilishi wa usalama katika shule zao. Hata hivyo, tunapendekeza saa za kufungua ziwe kati ya saa 08:00am na 3:30pm. Wanafunzi walio na wazazi au walezi ambao wana kazi muhimu za kijamii na wanafunzi walio katika hali mbaya pia watapokea programu na watalindwa. Sheria kuu ni kwamba uzuiaji wa maambukizi ndio kipaumbele bali na saa kamili za kufungua.

**Je, ikiwa saa za kufungua programu za kabla na baada ya shule (SFO) zitapunguzwa, karo pia itapunguzwa?**

Meneja wa Manispaa Eva Elisabeth Belboe: La, malipo ya mzazi yatabakia vile yalikuwa kabla ya kufunga shule na yatakuwa kulingana na kiwango kilichokubaliwa awali, saa za mtoto za kila wiki, bila kujali idadi ya saa ambazo programu inatoa sasa. Hata hivyo, ikiwa watoto watakuja na chakula chao cha mchana kwenye programu ya kabla na baada ya shule (SFO), ambacho tunawaulize wabebe katika wiki za kwanza, tutapunguza ada ya chakula.

**Je, huduma za mabasi/uchukuzi zinafanya kazi kama kawaida?**

Meneja wa Manispaa Eva Elisabeth Belboe: Naam, tumekuwa katika mazungumzo ya mara kwa mara na AtB kuhusu vile huduma za uchukuzi zitafanya kazi, na zitafanya kazi kama kawaida. AtB imeunda hati ya 'Maelezo ya uzuiaji wa maambukizi', ambayo inaelezea juhudi za kuzuia maambukizi katika huduma za uchukuzi shuleni. Hati hii pia inatoa mwongozo kwa shule, wazazi na walezi pamoja na madereva katika nyanja hii. Ninapendekeza usome hati hii.

**Ni kwa jinsi gani ambavyo siku ya shule itapangwa kuhusiana na uzuiaji wa maambukizi?**

Mwalimu Mkuu Trude Mathiesen: Mwongozo huu ambao tumepokea ni wazi na unatoa ushauri na miongozo mizuri. Sasa tuko katika shughuli ya kupanga watoto ili kuhakikisha kuwa uzuiaji wa maambukizi unafanyika. Shughuli hii inahusisha kupunguza vikundi hadi watu 15. Pia inahusisha hatua za usafi, na yule anayeweza kuhudhuria shule na yule hawezi. Shule zinatofautiana. Majengo, maeneo ya nje na maeneo yaliyo karibu yanatofautiana. Vifaa kama vyumba vya kubadilishia nguo na lavatori nk., zinatofautiana, na suluhisho basi zitatofautiana kulingana na shule. Hata hivyo, tunafuata ushauri na miongozo ambayo imepeanwa.

**Je, utawezaje kuweka watoto 15 kwa darasa moja na pia huweke nafasi ya mita 1?**

Mwalimu Mkuu Trude Mathiesen: Hili pia litatofautiana kulingana na shule. Katika Shule ya Ila tuna vifaa vidogo na vyembamba. Tutahitajika kuandaa na kupanga jambo hili kwa makini na kwa uangalifu sana. Sasa tumeanza kuondoa darasani vipengee vyote visivyo muhimu. Baadaye tutapanga madawati na kisha tutaona kuwa inawezekana. Ni vipengee muhimu pekee ambavyo tunaweza kuwa navyo darasani. Pia tunapendekeza shughuli nyingi za kufanya huko nje.

**Je, tunawezaje kuwa na uhakika kwamba walimu na wafanyakazi wasaidizi wataweza kusimamia watoto ili wasikaribiane sana wakati vikundi ni vikubwa hivi?**

Mwalimu Mkuu Trude Mathiesen: Hili ni jambo la mpangilio mwema na wa umakini. Kiwango cha kuwa makini ni kweli hakipimiki, lakini tutafikia. Kutakuwa na vikundi visivyobadilika na watu wazima wasiobadilishwa siku yote ya shule. Ni jambo la kupanga. Kwa mfano, watoto wote hawawezi kuwa nje kwa wakati mmoja.

**Je, mapumziko yatapangwa vipi? Je, kila mtu atakuwa nje wakati mmoja au katika vikundi?**

Mwalimu Mkuu Trude Mathiesen: Tutaweka mapumziko kwa vikundi. Shule kubwa zaidi ambazo zina maeneo makubwa zaidi kuliko yetu wanaweza labda kuweka makundi zaidi nje kwa wakati mmoja.

**Je, wazazi na walezi wanapaswa kuendeleaje ikiwa hatutaki kupeleka watoto wetu shuleni kabla ya likizo za majira ya joto?**

Mtaalam wa Saikolojia ya Kikliniki Torgunn Reitlo Malmo: Huenda kuna sababu tofauti za wazazi au walezi kutaka kuweka watoto wao nyumbani. Hii inajumuisha woga wa kuambukizwa, hali ya kuwa wamefutwa kazi au kuwa wana nafasi ya kufuatilia masomo ya nyumbani. Huenda mtoto amependa sana masomo nyumbani au anaweza kufanya kazi zaidi ya shule kuliko kawaida, au mtoto anaweza kuwa anatamani sana kurudi shuleni. Watoto wengine wanaweza kuhitaji mabadiliko zaidi ya kawaida na marekebisho kufuatia mapumziko ya muda mrefu mbali na shule. Ni muhimu wazazi na walezi kuwa na mazungumzo na shule kuhusiana na hili. Watoto wengi wanaweza kuguswa tofauti kuliko kawaida, katika hali ya athari kali au dhaifu za kihisia. Ni kawaida pia kwa watoto kutafuta starehe zaidi, msaada na ukaribu katika vipindi vya kutokuwa na uhakika wa karibu nao. Ni muhimu kwamba sisi watu wazima tuelewe na kukubali hili. Haichukuliwi kawaida kuwa mtoto wako anaogopa vitu sawa na wewe, na tunahitaji kusikia haswa kile wanaogopa. Watoto wanaweza pia kuathiriwa na kufadhaika kwa wazazi au walezi. Watoto huwa wanajua kile wazazi wao au walezi wanaogopa, na wanaweza pia kuwa na makosa katika kujua kwao.

**Je, watoto walio na wazazi au walezi katika kikundi cha walio hatarini waendele na masomo nyumbani?**

Afisa Mkuu wa Matibabu Betty Johanne Pettersen: Hii inategemea kuzingatia hali husika za kimatibabu. Kuna taratibu za kufuata katika hili, na inategemea ni aina gani ya ugonjwa ambao wazazi au walezi wanaugua na jinsi unavyodhibitiwa. Daktari anayetibu lazima awasaidie wazazi au walezi kufanya tathmini hii. Ikiwa ugonjwa umedhibitiwa vizuri na kutibiwa, mtoto anaweza kuhudhuria shule. Ikiwa ni suala la ugonjwa mbaya, mafundisho yaliyorekebisha, ikijumuisha masomo nyumbani, yanaweza kuzingatiwa na kuchanganuliwa kwa kushirikiana na shule.

**Je, tunahitaji barua ya ugonjwa kutoka kwa daktari ili kuweka mtoto wetu nyumbani wakati mmoja au zaidi ya wanafamilia wana pumu au magonjwa mengine ya msingi?**

Afisa Mkuu wa Matibabu Betty Johanne Pettersen: Ikiwa mtoto ana ugonjwa wa pumu na umedhibitiwa vizuri, mtoto anaweza kuhudhuria shule. Ikiwa wazazi au walezi wana ugonjwa mbaya na usiodhibitika, tunaweza kuanza mchakato wa kumzoesha mtoto. Kisha tutahitaji cheti cha matibabu.

**Je, sehemu za maeneo zitasafishwa mara ngapi na nani atawajibikia hili? Na vifaa vya kuchezea nk.? Je, vifaa vitaoshwa au kunyunyiziwa kiua vijidudu kabla na baada ya kutumika?**

Meneja wa Manispaa Eva Elisabeth Belboe: Mwongozo unasema mara 2-4 kwa kila siku ya shule, na huu ni ushirikiano kati ya wafanyakazi wanaosafisha na walioajiriwa shuleni na katika vituo vya utunzaji wa mchana. Wafanyakazi wanaosafisha wataosha kabisa vifaa vile na walioajiriwa pia watavipangusa. Wafanyakazi wanaosafisha wataosha kabisa sehemu zote za maeneo kila siku. Watoto walewale watapewa midoli ileile kwa kipindi fulani na

itasafishwa baada ya matumizi.

**Taratibu za kusafisha ni gani baada ya siku ya shule kumalizika? Na je, vifaa vyote vya shule na madawati, viti, mabENCHI, nk., zitaoshwa/ kunyunyiziwa viua vijidudu kabla ya siku ya shule inayofuata? Nani anawajibikia hili?**

Meneja wa Manispaa Eva Elisabeth Belboe: Mwongozo unasema kwamba wanafunzi watafuta madawati yao wenyewe. Wafanyakazi wanaosafisha watakuwa na vifaa katika hali safi kabla ya kuanza kwa shule. Shule pia inahusishwa moja kwa moja na wafanyakazi wanaosafisha na itakubaliana moja kwa moja nao ikiwa kitu kitatokea. Pia tunashirikiana vizuri na mkuu wa wafanyakazi wanaosafisha, na tutaweza kukamilisha hili.

**Je, shule inawezaje kudhibitisha kwamba mtoto wangu hataambukizwa COVID-19?**

Mtaalam wa Saikolojia ya Kikliniki Torgunn Reitlo Malmo: Kwa kweli ninaelewa hitaji la dhamana. Tunapoogopa, tunatafuta dhamana, tunataka kupunguza kutokuwa na uhakika ili tujihakikishie. Hata hivyo, kuna vitu vichache katika maisha ambavyo vinaweza kudhaminiwa. Hatuwezi kuhakikisha kwamba mtoto wako hataugua, licha ya ukweli kwamba kuna hatari ndogo sana kwa sababu ya hatua nzuri za kuzuia maambukizi.

Kumbuka! Wazazi na walezi pia wanahimizwa kuwasiliana na shule yao ikiwa wana maswali yoyote.